

## MASHUJAA WALETA MABADILIKO



# Sifa:

## Katuni Zaunganisha Mataifa: Mashujaa Waleta Mabadiliko

---

Hadithi - Josh Elder, Natabara Rollosson na Sean  
Southey

Sanaa - Grace Allison na Karl Kesel

Mchoraji wa picha - Type One International, Inc. -  
Amy Tookey

Tahariri - Josh Elder

Usanifu wa Kitabu - Ed Roeder

Tafsiri zimetolewa na Translation By Design

Mtafsiri wa Kiswahili - Boniface Kyalo

**Katuni Zaunganisha Mataifa: Heroes for Change** copyright © 2015 by Project Everyone, PCI Media Impact and Reading With Pictures.

Maelezo haya yanasambazwa bila malipo chini ya  
Leseni ya Kimataifa ya Creative Commons ya Sifa ya  
Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0.

Kwa maelezo zaidi:


<https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0>



# Jinsi ya Kusoma Kijitabu cha Katuni

**Maelezo mafupi** kwa kawaida huwa na masimulizi na wakati mwingine maandiko au maelezo mengine.

**Paneli** ni fremu ambazo kila moja ina sehemu moja ya hatua. Soma paneli kuanzia kushoto hadi kulia, juu hadi chini.




**Puto za Maneno** zina maneno ya mhusika. Mkia wa puto huelekeza kwa msemaji. Wakati mwingine rangi, maumbo, au fonti tofauti hutumiwa kuonyesha utu wa mhusika.

**Pambizo** ni nafasi kati ya paneli. Hapa ndipo msomaji lazima afikirie hatua kutoka paneli moja hadi paneli nyingine.

Polepole! Soma maandishi na picha kwa pamoja.  
Fikiria kuhusu kinachofanyika kati ya paneli.

HII NI DUNIA.  
KULINGANA NA SAYARI,  
DUNIA NI MUHIMU SANA.



NI DUNIA ILIYOJAA  
MAAJABU...

...YOTE NI YA ASILI..



...NA YALE AMBAYO  
SISI WENYWE  
TUMEYABUNU.



LAKINI HAKUNA CHOCHOTE  
DUNIANI KINACHOSTAAJABISHA  
SANA KAMA MABILIONI YA WATU  
WANAUIJUA KAMA MAKAO YAO.



KWA KUWA SISI  
WOTE TUNA KITU  
MAALUM NDANI  
YETU:

UMEZO WA KUWAZA  
DUNIA BORA NA  
KISHA KUCHUKUA  
HATUA HUIFANYA  
KUWA KWELI.



KWA HAKIKA HUO NI  
UMEZO MKUBWA.  
NA TUKITUMIA UMEZO  
HUO KUWASAIKIA  
WENGINE, SI HIYO  
INAWeza KUTUFANYA  
SISI WOTE...

KUWA MASHUJAA  
WA KIPEKEE?



JAMBO NZURI, KWA SABABU DUNIA  
INAHITAJI MASHUJAA WOTE  
INAYOWEZA KUPATA ILI KULINDA  
MAZINGIRA YAKE DHIDI YA MADHARA  
NA KUHAKIKISHA HAKI ZA BINADAMU  
KWA KILA MTU KWA KULINDA WATU  
WAKE DHIDI YA DHULUMA, UMASIKINI,  
NA KUKOSEKANA KWA USAWA.

LAKINI HAKUNA  
MTU YEYOTE -

HATA PIA SHUJAA  
WA KIPEKEE -


ANA NGUVU ZA  
KUTOSHA KUBEBA  
UZITO WA DUNIA  
PEKE YAKE.

LAKINI KWA PAMOJA, HIYO  
ITAKUWA HADITHI TOFAUTI.

KWA PAMOJA TUNAWEZA  
KUTATUA TATIZO LOLOTE NA  
KUSHINDA KARIBU  
CHANGAMOTO YOYOTE ILE.

TUNACHOHITAJI  
NI MPANGO.





HIYO NDIO MAANA UMOJA WA MATAIFA  
ULIZUNGUMZA NA ZAIDI YA WATU  
MILIONI 7 KATIKA NCHI 193 NA  
KUWAULIZA MAWAZO KUHUSU JINSI  
YA KUTATUA KILA KITU KABLA YA  
MWAKA 2030.

KATI YA MAMILIONI YA MAZUNGUMZO HAYO  
KULITOKEA MALENGO YA DUNIA KWA  
MAENDELEO ENDELEU -

MPANGO WA MAENDELEO YA KIUCHUMI,  
KIJAMII NA KIMAZINGIRA AMBAO UNAFIKIA  
MAHITAJI YA LEO BILA KUHATARISHA  
RASILIMALI ZA BAADAYE.

FIKIRIA KUHUSU MALENGO 17 YA DUNIA  
KAMA ORODHA KUU YA MAMBO YA  
KUFANYA KWA WATU NA SAYARI - NJIA  
YA SISI KUFANYA KAZI KWA PAMOJA ILI  
TUWEZE KUPATA SULUHISHO ZA  
MATATIZO YOTE MAKUBWA DUNIANI.



JINSI YA KUSOMA KIJITABU  
CHA KATUNI

HAITAKUWA RAHISI, LAKINI *INAWEZA*  
KUFANYIKA. NA IKWA MALENGO  
YATAFIKWA, ITAFANYA DUNIA KUWA  
MAHALI PENYE HAKI, UFANISI ZAIDI  
NA SALAMA ZAIDI KWA SISI WOTE.



MKUTANO MKUU WA UMOJA WA MATAIFA  
AMBAPO WAJUMBE WA TAIFA  
WANAKUTANA KUPITISHA MAAZIMIO



# MALENGO YA DUNIA

kwa Maendeleo Endelevu




LAKINI KUWEKA MALENGO NI MWANZO TU. NI WAJIBU WA KILA MMOJA KUCHUKUA HATUA NA KUHAKIKISHA ZIMEKAMILISHWA.


NA KILA MMOJA INAJUMUISHA WEEWE.

KWA HIYO UNASUBIRI NINI? PINDUA UKURASA ILI UNG'AMUE NI NINI UNACHOWEZA KUFANYA ILI KUSAIDIA!

# 1: JIFUNZE KUHUSU MALENGO HAYA.




NG'AMJIA MALENGO HAYO  
NI GANI NA UGUNDUE NI  
KWANINI NI YA MUHIMU KWA  
MAISHA YAKO MWENYEWI?



## 2: TANGAZIA KILA MTU

NJIA YA PEKEE AMBAYO MALENGO HAYO YANAWEZA KUFANIKIWA NI KUYAFANYA KUWA MAARUFU, KWA HIYO PATA NJIA BUNIFU ZA KUMTANGAZIA KILA MTU UNAYEMJUA KUHUSU MALENGO YA DUNIA NA UMHIMIZI AFANYE HIYO PIA!

#globalgoals inaweza kubadilisha dunia, lakini ikiwa tu sisi wote tutafanya kazi kwa pamoja!  
#tellevryone




# 3: FANYA JAMBO



HUSIKA NA MASHIRIKA  
AMBAYO YANASHUGHULIKIA  
MATATIZO AMBAYO NI  
MUHIMU SANA KWAKO,  
HUSIKA NA SERIKALI YAKO  
NA UTAFAUTE NJIA ZA KUWA  
SHUJAA WA MABADILIKO  
KATIKA JAMII YAKO  
MWENYEWI!





KWA SABABU SUALA NI HILI: SISI  
WOTE TUNA SIFA MAALUM, UWEZO WA  
KIPEKEE WA KUSAIDIA KUBADILISHA  
SAYARI YETU – NA JINSI TUNAVYOISHI –  
ILI KUWA BORA ZAIDI.

KWA HIIYO TAFUTA  
UWEZO WAKO WA  
KIPEKEE NA UUSHIRIKI  
NA DUNIA!

NA KWA PAMOJA  
TUTAKAMILISHA  
MAAJABU!

# MASHUJAA WALETA MABADILIKO

World Largest Lesson ni mradi wa kushirikiana wa elimu unaounga mkono tangazo la Malengo ya Ulimwengu ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu. Mradi huu ni thibitisho tosha kuhusu umuhimu wa Malengo 17 ya Ulimwengu "Ushirikiano wa Malengo" na haungewezekana bila msaada wa washirika wetu wote wanaofanya kazi na sisi na wenyewe kwa wenyewe.

Asante kwa Timu yetu ya Uanzilishi:

---



PEARSON



Imedhaminiwa Na:



Imesambazwa Na:



Imetafsiriwa Na:



Shukrani maalum kwa wale waliofanya kazi na sisi duniani kote:

---



Mipango ya masomo imeundwa kwa kushirikiana na Think Global [www.think-global.org.uk](http://www.think-global.org.uk). Kukuza masomo kwa ulimwengu wa haki na endelevu.

---



Swahili (Kiswahili)

